

WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS



MFUKO WA FAIDA (FAIDA FUND)



(FAIDA FUND)

(Mfuko Endelevu wa Kukuza Uwekezaji)

WARAKA WA TOLEO

KWA UFUPI

Vipande vitauzwa kwa bei ya Sh. 100 kwa kila kipande wakati ya mauzo ya awali na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi.

Tarehe ya Ufunguzi ya mauzo ya mwanzo: 01 Novemba, 2022

Tarehe ya Kufungwa kwa Mauzo ya Mwanzo: 30 Disemba, 2022

Waraka huu unaeleza kwa ufupi, habari kuhusu Mfuko wa Faida. Mwekezaji mtarajiwa anapaswa kusoma waraka huu kabla ya kuwekeza. □ Waraka huu utunzwe kwa marejeo ya baadaye.

Maelezo ya Mfuko yameandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 ya mwaka 1997 (kama ilivyorekebishwa) na Kanuni zinazosimamia Soko la Mitaji (Uwekezaji wa Pamoja), Gazeti la Serikali Na.770 la mwaka 1997. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana haijaruhusu au kukataza kuuzwa kwa viapnde vya Mfuko huu.

Wawekezaji watarajiwa, wanapaswa kuwa waangalifu katika kutafakari mambo yaliyoelezwa chini ya Ibara ya “Hatari za Uwekezaji” (Risk Factors).

Waraka huu utaendelea kutumika hadi hapo mabadiliko yatakapotokea na mabadiliko hayo yatawasilishwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa ajili ya kupitishwa kabla ya kusambazwa kwa wenyevipande

TAHADHARI

**KAMA UNA MASHAKA KUHUSIANA NAYALIYOMO KATIKA
WARAKA HUU, UNAPASWA KUMUONA DALALI**

**WAKOWA SOKO LA HISA, MENEJA WA BENKI, MWANASHERIA,
MHASIBU AU MSHAURI MWINGINE WA MAMBOYA UWEKEZAJI**

**BEL/THAMANI HALISI YA VIPANDE VYA MFUKO WA FAIDA PAMOJA
NA MAPATO KUTOKA KWENYE VIPANDE INAWEZA KUONGEZEKA
AU KUPUNGUA.**

DONDOO ZA MFUKO WA FAIDA

S/n	Dondoo	Maelezo
1.	Madhumuni	<ul style="list-style-type: none"> Mfuko huu ni mpango ulio wazi unaotoa fursa nyingine ya uwekezaji kwa Watanzania hasa wa kipato cha kati na cha chini kupitia uwekezaji katika vipande ili kupata mapato shindani kupitia ukuaji wa mitaji. Kutengeneza utamaduni wa kuwekeza katika Masoko ya Fedha na Mitaji.
2.	Aina ya Mfuko	Ni Mfuko wa uwekezaji wa pamoja unaotoa fursa ya uwekezaji unaokua pamoja na kujitoa katika uwekezaji pasipo na gharama yoyote
3.	Nani Anar uhusi- wa Kuwekeza	Mfuko huu uko wazi kwa Watanzania na Wakazi waliopo ndani na nje ya nchi, unahusisha watu binafsi (ikijumuisha watoto), na wawekezaji wasio watu binafsi kama Mifuko ya Pensheni, Mabenki/Mashirika Taasisi za serikali, Mamlaka za Udhibiti, Vyombo vya ulinzi na usalama, Asasi zisizo za kiserikali na Mashirika mengineyo n.k.
4.	Sarafu ya Msingi	Aina ya Fedha itakayotumika ni Shilingi ya Kitanzania (Tsh.) tu.

5.	Kiwango cha chini cha uwekezaji	<p>Kiwango cha Uwekezaji itakuwa kama ifuatavyo:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kiwango cha Awali cha Uwekezaji ni kuanzia Tsh 10,000/= • Mauzo yanayofuata baada ya mauzo ya awali ni kuanzia Tsh 5,000/=
6.	Kiwango cha juu cha Uwekezaji	Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza.
7.	Matumizi ya Fedha za Uwekezaji	Fedha hizo zitawekezwa kwenye Masoko ya Fedha na Mitaji yenye kiwango cha chini cha hatari za uwekezaji.
8.	Umiliki wa Vipande	Umiliki wa mtu mmoja na umiliki wa pamoja unaruhusiwa katika mfuko huu. Hata hivyo, umiliki wa pamoja hauzihusu taasisi/kampuni.
9.	Thamani ya kipande	Thamani ya mwanzo ya kipande ni Tsh 100/=. Hii itatumika wakati wa mauzo ya awali na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi.
10.	Uwazi	Mfuko utangaza thamani halisi ya kwanza ya mfuko (Net Asset Value) katika kipindi kisichozidi siku 10 za kazi tangu kufungwa kwa mauzo ya awali na baadaye itatathimini na kutangaza kila siku ya kazi.
11.	Ukwasi	Uuzaji wa vipande utafanyika kila siku baada ya mienzi mitatu tangu kumalizika kipindi cha mauzo ya awali. Mfuko utatuma malipo ya mauzo ya vipande ndani ya siku tatu za kazi baada ya kupokea maombi. katika Makao Makuu ya Watumishi Housing Investments. Fedha za mauzo zitatumwa moja kwa moja katika akaunti ya benki ya mwekezaji au simu ya mkononi iliyosajiliwa.

FAIDA FUND

12.	Tozo la kujiunga na kujitoa:	Mwekezaji hatotozwa gharama yeyote ya kujiunga au kujitoa katika mfuko
13.	Sera ya Uwekezaji	Mfuko utawekeza katika masoko ya fedha kwa asilimia 100%. Kiwango cha uwekezaji katika masoko ya fedha na Dhamana kitalenga kupata mapato makubwa katika soko.
14.	Kigezo	Kiwango cha riba cha Hati Fungani za Serikali za miaka mwili.
15.	Ulinzi wa mtaji:	Lengo kuu ni kulinda mtawanyo wa uwekezaji ili kutoathiri thamani ya vipande huku mtazamo mkuu ukiwa ni kipato kinachotokana na riba bila hatari zisizokuwa na ulazima.
16.	Muda wa kuendesha Mfuko	Mfuko huu ni wa kudumu kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano.
17.	Faida za Kikodi	Kwa mujibu wa sheria za nchi, mgawanyo wa mapato ya Mfuko yamesamehewa kodi ya mapato kwa wawekezaji.

MFUKO WA FAIDA (FAIDA FUND)

(Umeidhinishwa kwa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

<p>Sponsor, Manager and Investment Advisor</p>  <p>Watumishi Housing Investments Golden Jubilee Towers, 4th Floor, 7 Ohio Street/Kibo Street, P.O.Box 5119, 11481 Dar es Salaam</p>	<p>Custodian</p>  <p>CRDB Bank PLC Head Office, Azikiwe Street P.O.Box 268, Dar es Salaam</p>
<p>Auditors</p>  <p>Controller & Auditor General National Audit Office, 4 Ukaguzi Road, P.O.Box 950, Hazina Street, 41104 Dodoma</p>	<p>Registrar</p>  <p>Watumishi Housing Investments Golden Jubilee Towers, 4th Floor, 7 Ohio Street/Kibo street, P.O.Box 5119, 11481 Dar es Salaam</p>
<p>Advocates</p>  <p>ABENRY & Company Golden Jubilee Towers, 3rd Floor, Main Tower, Ohio Street/Kibo Street, P.O.Box 3467, Dar es Salaam</p>	<p>Lead Advisor</p>  <p>SOLOMON Stockbrokers Limited</p> <p>SOLOMON Stockbrokers Ltd PSSSF House, Ground Floor Samora Avenue/Morogoro Road Box 77049, Dar es Salaam</p>

Wajumbe wa Bodi ya Watumishi Housing Investments, ambao majina yao yameorodheshwa hapa chini wanakubali kuwajibika kwa taarifa zilizomo katika Waraka huu kwamba ni sahihi wakati wa tarehe ya kutolewa kwa waraka.

Majina ya Wajumbe wa Bodi

Bw.Hosea Kashimba	-	Mwenyekiti
Bw.Masha Mshomba	-	Mjumbe
Bw.Bernard Konga	-	Mjumbe
Bw.Nehemia Kyando Mchechu	-	Mjumbe
Bw.Shabani Mande	-	Mjumbe
Bi.Agnes Meena	-	Mjumbe
Dk.Fred Msemwa	-	Katibu

Yaliyomo

1. UTANGULIZI	1
2. MUUNDOWA MSIMAMIZI.....	3
3. USIMAMIZIWA MFUKO WA FAIDA.....	4
4. MAJUKUMUYA MSIMAMIZI.....	5
5. MWANGALIZI WA MFUKO.....	6
6. TAMKO LA MSIMAMIZI KUZINGATIA SHERIA.....	10
7. GHARAMA ZA TOLEO LA KWANZA.....	11
8. HATARI ZA UWEKEZAJI.....	11
9. MAELEZO YA TOLEO YA MFUKO - SIFA ZA MFUKO.....	13
9.2. RATIBAYA MAUZO YA AWALI.....	13
10. MASHARTIYA KUJIUNGA NA MFUKOWA FAIDA.....	19
11. SERA YA UWEKEZAJI (INVESTMENT POLICY).....	19
12. KUWEKA REHANIVIPANDE KAMA DHAMANAYA MKOPO.....	20
13. KUBADILISHA/KUHAMISHAWAMILIKIWA VIPANDE.....	21
14. MAUZO YA VIPANDE (ALLOTMENT OF UNITS).....	21
15. TAARIFA YA AKAUNTI (SOA).....	22
16. UTEUZI WA MWAKILISHI/MRITHI.....	22
17. UNUNUZI WA VIPANDE.....	24

18. MAUZOYANAYOFUATA NA UUZAJI WA VIPANDE KWA MSIMAMIZI.....	26
19. MASHARTIYA UWEKEZAJI KWA WASHIRIKA.....	29
20. MAONI NA MALALAMIKO YA WAWEKEZAJI.....	29
21. GHARAMA ZA MFUKO.....	31
22. JINSIYA KUTATHMINI THAMANI HALISIYA MFUKO.....	32
23. HAKI ZA WAMILIKI WA VIPANDE.....	33
24. KODI.....	35
25. UKOMO KWA MFUKO.....	36
26. MAMBO YA JUMLA.....	36
27. MIKUTANO.....	37
KIAMBATISHI NA.....	38
SEHEMU YA KWANZA MAELEZO YA JUMLA.....	41

1.0. UTANGULIZI


Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing (WHI) lililoanzishwa tarehe 6 Februari mwaka 2013 chini ya Sheria ya Makampuni Sura Na. 212 ya mwaka 2002. WHI iko chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Majukumu yake ni kama ifuatavyo:

- a) Kuanzisha na Kusimamia Mifuko ya Uwekezaji wa pamoja nchini.
- b) Kutekeleza Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma (Public Servants Housing Scheme) pamoja na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii.
- c) Usimamizi wa majengo (milki)
- d) Kutoa huduma za ujenzi pamoja na huduma za ushauri wa majenzi.


1.2. KAZI ZA MSIMAMIZI

Kulingana na majukumu yake, WHI hadi sasa imeshaanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa pamoja katika milki (Watumishi Housing REIT). Mfuko huu ulianzishwa tarehe 21 Novemba 2014 kwa ajili ya kukuza mitaji katika uendelezaji wa milki na kujenga Nyumba za gharama nafuu za makazi na biashara. Wawekezaji katika Mfuko huu ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Mfuko wa Watumishi Housing REIT una mtaji unaofikia kiasi cha Tsh 59.65 bilioni kupitia wawekezaji wake. Thamani halisi ya Mfuko kwa miaka iliyopita hadi June 2021 imeoneshwa hapa chini.



Thamani halisi ya Mfuko kwa kipande imeongezeka kutoka Tsh 250 mwaka 2015 hadi Tsh 317 mwaka 2021.



1.3. MCHAKATO WA KUENZISHA MFUKO WA FAIDA

Mpaka sasa WHI imeanzisha Mfuko wa WHI-REIT ambao malengo yake makubwa ni kuwekeza katika milki. Hata hivyo, mfuko wa WHI-REIT kulingana na sifa zake umetoa fursa kwa uwekezaji wa muda mrefu. Pia Mfuko huu una kipindi cha zuio la kujitoa (Lock-in-period). Hivyo basi, Mfuko hautoi fursa kwa wawekezaji kujiunga na kuwekeza kwa muda mfupi.

WHI imeona kuna uhitaji wa haraka wa kuitumia fursa za taasisi na watu binafsi wenye kipato kikubwa, cha kati na cha chini kwa kuanzisha Mfuko wa Faida utakaokidhi mahitaji yao huku ukiwapatia faida kubwa bila gharama ya kujitoa.

2. MUUNDO WA MSIMAMIZI

WHI inasimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeundwa na Wakurugenzi Wakuu kutoka Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mkurugenzi huru kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mwingine kutoka Kampuni ya Mikopo ya Nyumba (TMRC). Bodi inasaidiwa na Kamati zake ambazo ni Kamati ya Fedha na Uwekezaji na Kamati ya Ukaguzi na Vihatarishi. Mkurugenzi Mtendaji pia ni Katibu wa Bodi na ndiye mwendeshaji wa majukumu ya kila siku ya WHI.

2.1. Majukumu ya Bodi

Majukumu ya Bodi ni pamoja na:

- a) Kufanya maamuzi kuhusu mipango ya Uwekezaji yenye lengo la kuongeza Faida au thamani ya rasilimali za Shirika.
- b) Kuanzisha na kuendesha Mifuko ya Uendeshaji wa pamoja katika njia ambayo itaongeza thamani ya Mifuko.
- c) Kuhakikisha kuna mifumo ya udhibiti wa ndani, utawala bora na usimamizi wa vihatarishi.

3. USIMAMIZI WA MFUKO WA FAIDA

Mfuko wa FAIDA iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Mitaji na Masoko (CMSA), utasimamiwa na Watumishi Housing Investments (WHI). Bodi ya Wadhamini imeunda muundo wa utendaji ili kutekeleza majukumu ya kila siku ya Mfuko huu.

3.1. BODI YA WADHAMINI YA WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

Na.	Jina	Nafasi	Uraia
i	Bw. Hosea Kashimba	Mwenyekiti	Mtanzania
ii	Bw. Masha J. Mshomba	Mdhamini	Mtanzania
iii	Bw. Bernard Konga	Mdhamini	Mtanzania
iv	Bw. Nehemia Kyando Mchechu	Mdhamini	Mtanzania
v	Bw. Shabani Mande	Mdhamini	Mtanzania
vi	Bi. Agnes Meena	Mdhamini	Mtanzania
vii	Dkt. Fred Msemwa	Katibu	Mtanzania

3.2. MENEJIMENTIYAWHI

Menejimenti ya Watumishi Housing Investments ni kama ifuatavyo:

Na.	Jina	Nafasi	Uraia
i	Dkt. Fred Msemwa	Mkurugenzi Mtendaji	Mtanzania
ii	Bw.Paskali Massawe	Mkurugenzi wa Fedha na Utawala	Mtanzania
iii	Bw.Sephania Solomon	Mkurugenzi Mwendeshaji	Mtanzania
iv	Bw.Joel Maeda	Mkuu wa Kitengo cha Sheria	Mtanzania
v	Mha. Lwitiko Mwandobo	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi	Mtanzania
vi	Bw.Raphael Mwabuponde	Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano	Mtanzania
vii	Yonas Mtana	Mkuu wa Kitengo cha Uk-aguzi	Mtanzania

4. MAJUKUMUYA MSIMAMIZI

Majukumu ya Msimamizi ni kama ifuatavyo:

- a) Kusimamia na kulinda maslahi ya Wawekezaji kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano pamoja na sheria nyingine zinazohusika;
- b) Kutunza vitabu na kumbukumbu za mfuko pamoja na kuandaa hesabu na taarifa zinazohitajika;
- c) Kuchapisha na kusambaza taarifa ya mwaka kwa Wawekezaji wa Mfuko ndani ya kipindi cha miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha. Kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko na Mitaji, Msimamizi anaweza kusambaza taarifa fupi kwa wawekezaji.

- d) Kutunza kumbukumbu za wawekezaji wa Mfuko;
- e) Kuhakikisha kuwa kuna mifumo imara na taratibu rafiki za kuwahudumia wawekezaji wa Mfuko;
- f) Kuhakikisha kuwa Waraka wa Makubaliano unapatikana muda wowote wa saa za kazi kwa ukaguzi kwa mtu yeyote bila gharama au gharama nafuu iwapo nakala itahitajika.

5. MWANGALIZIWA MFUKO

5.1. MUUNDO WA MWANGALIZI

Mwangelizi wa Mfuko ni CRDB Bank PLC ambayo ni Benki ya Biashara iliyoruhusiwa kuendesha Biashara chini ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991. CRDB Bank PLC ni Benki ya Umma iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 1996, Cheti cha Usajili Na. 30227. Wanahisa wa CRDB Bank PLC ni Watanzania mmoja mmoja na Mashirika ya ndani na nje ya Nchi ikiwemo Shirika la DANIDA. CRDB ni moja ya Benki inayokua kwa kasi nchini Tanzania. Ofisi yake iliyoandikishwa nchini ipo Barabara ya Bibi Titi Mohammed, S.L.P 268, Dar es Salaam.

Benki ya CRDB ni Mwangelizi wa Mfuko wa Faida ambao umeidhinishwa na Mamlaka ya Mitaji na Masoko (CMSA) ili kuweza kufanya uangalizi wa mifuko ya uwekezaji Tanzania.

5.2. BODIYA WAKURUGENZIYA MWANGALIZI

Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB Bank Plc inaundwa na wajumbe wafuatao:

No.	Jina	Nafasi	Uraia
i)	Bw. Ally Hussein Laay	Mwenyekiti	Mtanzania
ii)	Bw. Abdulmajid Mussa Nsekela	Mkurugenzi Mtendaji	Mtanzania
iii)	Mha. Boniface C. Muhegi	Mjumbe	Mtanzania
iv)	Bw. Hosea Ezekiel Kashimba	Mjumbe	Mtanzania
v)	Dk. Fred Msemwa	Mjumbe	Mtanzania
vi)	Bw. Royal John Lyanga	Mjumbe	Mtanzania
vii)	Bw. Gerald Paul Kasaato	Mjumbe	Mtanzania
viii)	Prof. Neema Munisi Mori	Mjumbe	Mtanzania
ix)	Bw. Jes Klausby	Mjumbe	Mtanzania
x)	Prof. Faustine Karrani Bee	Mjumbe	Mdenishi
xi)	Bw. Martin Steven Warioba	Mjumbe	Mtanzania
xii)	Bw. Abdul Ally Mohamed	Mjumbe	Mtanzania
xiii)	Bi. Naiman Miranda	Mjumbe	Mtanzania

5.3. MENEJIMENTIYA MWANGALIZI

Na.	Jina	Nafasi
i)	Bw. Abdulmajid Mussa Nsekela	Mkurugenzi Mtendaji
ii)	Bw. Fredrick Bayona Nshekanabo	Afisa Mkuu wa Fedha
iii)	Bw. Bruce Mwile Mwasenga	Afisa Mkuu Uendeshaji
iv)	Bw. John Baptist Rugambo	Katibu wa Kampuni
v)	Bw. Alexander Samson Ngusaru	Mkurugenzi wa Hazina
vi)	Bi. Tully Esther Mwambapa	Mkurugenzi wa Mahusiano ya Umma
vii)	Bw. James Isaack Mabula	Mkurugenzi wa Idara Hatarishi
viii)	Bw. Wilson Mzava	General Manager, CIB Insurance Broker
ix)	Bw. Leslie S James Mwaikambo	Mkurugenzi Uendeshaji wa Benki
x)	Bw. Boma Raballa	Mkurugenzi Wateja Wadogo na wa Kati
xi)	Bw. Pendason Philemon	Mkurugenzi wa Manunuzi
xii)	Bw. Xavery Makwi	Mkurugenzi wa Mikopo
xiii)	Godfrey Rutasingwa	Mkurugenzi wa Rasilimali Watu
xiv)	Bw. Leo P. Ndimbo	Mkurugenzi Mabadiliko ya Kibiashara
xv)	Bw. Deusdedit Pastory Massuka	Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
xvi)	Bw. Prosper Gunze Nambaya	Mkurugenzi Wateja Wakubwa
xvii)	Bw. Godfrey Nimrod Sigalla	Mkurugenzi Ukaguzi wa Ndani

5.4. KAZI ZA MWANGALIZI

Kazi za mwangalizi zimeelezwa katika sheria na pia katika Waraka wa Makubaliano wa Mfuko. Kazi hizo ni pamoja na:

- (a) Kusimamia na kuhakikisha Usalama wa mali za Mfuko kulingana na matakwa ya Waraka wa Makubaliano na kuhakikisha fedha na mali zimesajiliwa kwa maelekezo ya Mfuko;
- (b) Kuwajibika kwa makosa yoyote yaliyofanywa na Wakala yeyote ambaye amekabidhiwa mali ya Mfuko kama vile ni makosa ya mtu aliyeteuliwa naye kuhusiana na uwekezaji uliofanywa;
- (c) Kuchukua hatua madhubuti kuhusiana na mauzo ya vipande au kusitisha, kutegemeana na masharti kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano;
- (d) Kuhakikisha kwamba njia zinazotumiwa na Msimamizi kukokotoa thamani ya vipande ni sahihi na kwamba bei ya uuzaji na ununuzi wa vipande zinakokotolewa kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano;
- (e) Kutekeleza maagizo ya Msimamizi kuhusiana na uwekezaji isipokuwa kama yatapingana na masharti ya Waraka wa Makubaliano;
- (f) Kuhakikisha kwa uangalifu kuwa ukomo wa uwekezaji na mikopo kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Makubaliano na sheria na taratibu nyingine zinazohusu uendeshaji wa Mfuko huu zinazingatiwa;
- (g) Kwa maoni yake kutoa taarifa kwa wawekezaji ambayo itajumuishwa katika taarifa ya mwaka ya Mfuko ili kuonesha kwamba Msimamizi amesimamia Mfuko kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano. Iwapo kuna kasoro zilizojitokeza, zitajwe na hatua zilizochukuliwa;

- (h) Kuchukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa hati ya umiliki wa vipande inatolewa endapo fedha za uwekezaji zimepokelewa na Msimamizi wa Mfuko;
- (i) Kuhakikisha kwamba mali mbalimbali za uwekezaji zinasajiliwa kwa jina la Mfuko na;
- (j) Pale ambapo uwekezaji umehifadhiwa katika Mfumo wa Kielektroniki, basi Msimamizi atahakikisha rasilimali hizo zimewekwa kwa utaratibu unaotengenisha mali za Msimamizi na mali za Mfuko.

6. TAMKO LA MSIMAMIZI KUZINGATIA SHERIA

Inathibitishwa kwamba:

- (a) Waraka wa Toleo hili uliotumwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ni kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 kama ilivyorekebishwa na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Uwekezaji wa Pamoja) za mwaka 1997.
- (b) Mahitaji yote ya kisheria, taratibu na maagizo yaliyotolewa na Serikali na mamlaka zinginezo katika kuanzisha Mfuko wa Faida zimezingatiwa.
- (c) Maelezo yaliyotolewa ndani ya Waraka huu ni ya kweli na ya kutosha kumwezesha mwekezaji kufanya uamuzi wa busara kuwekeza katika Mfuko huu.

Dk Fred Msemwa
Mkurugenzi Mtendaji
Mahali: Dar es Salaam

Imetiwa sahihi na Mkurugenzi Mtendaji

7. GHARAMA ZA TOLEO LA KWANZA

Gharama za kuanzisha Mfuko wa Faida ni kama ifuatavyo:-

- a) Gharama za matangazo, masoko na elimu kwa umma
- b) Gharama za Mshauri Mwelekezi
- c) Gharama za Uchapishaji na Posta
- d) Gharama za Huduma za Wanasheria na Wakaguzi wa Hesabu
- e) Gharama nyinginezo.

Gharama hizi za Toleo la Kwanza zitalipwa na Watumishi Housing Investments ambaye ni Mdhamini na Msimamizi wa Mfuko na hakutakuwa na gharama za ziada kwa mwekezaji anayeingia kwenye mfuko.

8. HATARI ZA UWEKEZAJI

Mwekezaji anapaswa kutambua kwamba, uwekezaji wa rasilimali za Mfuko unakabiliwa na hatari mbalimbali zinazoweza kuathiri hali ya Mfuko siku hadi siku, hivyo kuweza kusababisha kupanda au kushuka kwa thamani halisi ya Mfuko kutegemea uwekezaji. Hata hivyo, utendaji wa miaka iliyopita sio kiashiria muhimu kwa mafanikio ya baadaye ya Mfuko.

Wawekezaji sharti watambue, miongoni mwa mambo mengine kwamba:

- a) Mbali na dhamana za serikali, dhamana zingine zilizotolewa na makampuni ya sekta binafsi, zinaweza kushindwa kulipa deni. Kutambua hilo, Msimamizi wa Mfuko amejipanga kuwekeza kwenye Hati Fungani mbalimbali za Serikali zenye mapato yasiyobadilika ili kupunguza/kuondoa hatari za uwekezaji.
- b) Mabadiliko ya viwango vya riba vinaweza kuathiri thamani ya dhamana zenye mapato yasiyobadilika ambazo zimewekezwa na Mfuko. Ili kukabiliana na hatari hii, Msimamizi atawekeza katika Hati Fungani ambazo zitaiva kwa vipindi tofauti na Amana za muda maalumu za vipindi tofauti.
- c) Mabadiliko katika viwango vya kubadili fedha yanaweza kuathiri thamani ya rasilimali za Mfuko katika dhamana zilizo katika fedha za kigeni (hapo Serikali itakaporuhusu Mfuko kuwekeza nje ya nchi). Mfuko wa Faida utaweza kuondoa hatari hii kwa kuweka utaratibu wa kufanya uwekezaji kwa kutumia sarafu ya Tanzania. Kwa maana nyingine Mfuko hautaruhusu uwekezaji kutumia sarafu ya nje.
- d) Utaratibu wa kodi zinazotowazwa katika mapato ya dhamana za uwekezaji unaweza kubadilika, hivyo kuathiri mapato ya Mfuko pamoja na mapato kwa mwekezaji. Mfuko wa Faida utapunguza hatari hii kwa kutumia wataamu wa masuala ya kodi ambao watatoa maelekezo kwa wawekezaji kuhusiana na mabadiliko ya kodi yanayoweza kuathiri uwekezaji wao.

- e) Mabadiliko yeyote kwenye sheria/kanuni yanaweza kuathiri utendaji wa Mfuko. Msimamizi wa Mfuko huu atazingatia sheria na kanauni za nchi na Mamlaka za Udhibiti kama vile CMSA, Benki Kuu ya Tanzania. Msimamizi atatekeleza mabadiliko yoyote ya sheria/kanuni na kuwataarifu wawekezaji athari za mabadiliko ya sheria/kanuni katika uwekezaji.
- f) Mazingira mengine yasiyoweza kutabirika yanaweza kuathiri uwekezaji ambao Mfuko wa Faida umewekeza na hivyo kuathiri mtiririko wa thamani ya kipande. Msimamizi wa Mfuko atafuatailia kwa karibu mwenendo wa soko katika uwekezaji ili kupunguza hatari zinazoweza kujitokeza.

9. MAELEZOYA TOLEOYA MFUKO - SIFA ZA MFUKO

9.1. MFUKO WA FAIDA

Mfuko wa Faida umelenga kutoa fursa mbadala ya uwekezaji kwa wawekezaji wa taasisi kubwa, wawekezaji wenye kipato cha kati na cha chini kwa kuwekeza pesa zao za ziada kwa kipindi cha muda mfupi na muda wa kati huku wakipata viwango vizuri/shindani vya faida.

9.2. RATIBAYA MAUZOYA AWALI

Ratiba ya mauzo ya awali ya vipande vya Mfuko wa Faida kwa Umma:

- a) Mauzo ya awali: 01 / 11 / 2022
- b) Mwisho wa mauzo ya awali: 31 / 12 / 2022

- c) CMSA kuidhinisha orodha ya wawekezaji 05 / 01 / 2023
- d) Mgawanyo wa vipande: 10 / 01 / 2023
- e) Ufunguzi rasmi 14 / 01 / 2023
- f) Mauzo na Manunuzi ya vipande 10 / 01 / 2023
- g) Kuanza Ununuzi wa vipande (Repurchase) 01 / 04 / 2023

Kumbuka: Kwa namna yoyote ile kipindi cha mauzo ya mwanzo hakitaongezwa kwa sababu inaweza kuleta athari kwa wawekezaji kukosa imani na kuathiri maendeleo ya soko.

9.3. AINAYA MFUKO

Mfuko huu ni mfuko wa wazi wenye kukua, hatari ndogo za uwekezaji na kiwango kikubwa cha ukwasi.

9.4. MALENGOYA MFUKO

- a) Mfuko unatoa fursa mbadala ya uwekezaji kwa wawekezaji wakubwa, wa kati na wa chini; iwe taasisi au mtu binafsi kwa kuwekeza fedha zao za ziada kwa kipindi cha muda mfupi au muda wa kati huku wakipata riba nzuri/shindani.
- b) Kukuza utamaduni wa uwekezaji katika masoko ya fedha.
- c) Hatari ndogo za uwekezaji na kiwango kikubwa cha ukwasi ni sifa ya uhakika ya mfuko huu. Lengo kuu ni kuulinda uwekezaji na hatari

za kupungua kwa thamani, ukilenga kupata mapato yatokanayo na riba pasipo hatari kubwa zisizo za lazima

9.5. NANI ANAWEZA KUWEKEZA

Mfuko uko wazi kwa uwekezaji kwa:

- a) Watanzania wakazi na wasio wakazi au nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki kwa umiliki wa mtu mmoja mmoja (ikijumuisha watoto) au umiliki wa pamoja.
- b) Wazazi au walezi kwa niaba ya watoto Watanzania wakazi au wasio wakazi au wa Afrika Mashariki ambao hawajatimiza umri wa mtu mzima.
- c) Makampuni au taasisi zilizosajiliwa Tanzania au ndani ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. d) Serikali za mitaa.
- e) Mifuko ya Pensheni iliyoanzishwa Tanzania au katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- f) Vyama vya Ushirika, vyama vya wafanyakazi, mashirika ya misaada au mashirika ya dini, asasi nyingine za kiraia pamoja na vyama vya uwekezaji vilivyosajiliwa Afrika Mashariki;
- g) Watu binafsi/taasisi/makampuni kama itakavyoamuliwa na WHI kwa kuzingatia sheria na kanuni za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

9.6. KIWANGO CHA CHINI/JUU CHA UWEKEZAJI

- a) Kiwango cha Awali cha Uwekezaji ni kuanzia Tsh 10,000/=
- b) Mauzo yanayofuata baada ya mauzo ya awali ni kuanzia Tsh 5,000/=
- c) Hakutakuwa na kiwango cha juu cha uwekezaji kama ilivyoelekezwa kwenye Waraka wa Toleo, hivyo mwekezaji atauziwa vipande kulingana na uwekezaji wake.

9.7. UMILIKI WAVIPANDE

Umiliki wa mtu mmoja na umiliki wa pamoja unaruhusiwa katika mfuko huu. Hata hivyo, umiliki wa pamoja hauzihusu taasisi/kampuni.

9.8. THAMANIYA KIPANDE

Thamani ya mwanzo ya kipande ni Tsh 100/=. Hii itatumika wakati wa mauzo ya awali na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi.

Kumbuka: Mfuko huu utakuwa wazi kwa mauzo na ununuzi wa vipande baada ya kipindi cha mauzo ya awali.

9.9. AINAYA UWEKEZAJI

Mfuko huu ni mfuko wa kukuza mtaji usio kuwa na gharama zozote zinazotowwa kwa mwekezaji wakati wakuingia wala kutoka.

9.10. GHARAMA ZA KUINGIA

- a) Vipande vitauzwa ama kugawiwa kwa wawekezaji bila gharama yoyote

ya kuingia katika mfuko (Entry Load).

- b) Wakati wa mauzo ya mwanzo, vipande vitagawiwa vikiwa na thamani ya shilingi 100 kwa kila kipande. Hata hivyo, kwa mauzo yanayofuata (subsequent sale) vipande vitagawiwa vikiwa na thamani halisi ya kipande kwa kipindi hicho (prevailing applicable Net Asset Value).

9.11. GHARAMA ZA KUJITOA KWENYE MFUKO

Mwekezaji anaweza kuuza vipande vyake kwa thamani halisi ya kipande kwa wakati wa kuuza (prevailing applicable Net Asset Value). Hakutakuwa na tozo lolote kwa mwekezaji anayejitoe kwenye mfuko.

9.12. UKWASI – UNUNUZI WAVIPANDE

Moja ya majukumu ya Mfuko ni kutoa Ukwasi wa kiwango cha juu kwa wawekezaji wake kwa masharti yafuatayo:

- a) Ununuzi wa vipande utafanyika kipindi chote cha mwaka. Ununuzi wa vipande katika Mfuko utanza baada ya kumalizika kwa kipindi cha mauzo ya awali.
- b) Msimamizi atakamilisha ununuzi wa vipande ndani ya siku tatu baada ya kupokea maombi.

c) MAMBO MUHIMU:

- i) Fedha zitakazopatikana kwenye manunuzi zitawekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mmiliki wa vipande au kupitia namba ya

simu ya mkononi iliyosajiliwa.

- ii) Wawekezaji watapewa chaguo la kutuma maombi ya uuzaji wa vipande kwa njia ya kielektroniki (kutuma maombi mtandaoni kupitia Tovuti ya WHI au simu za mkononi) au kutuma fomu ya nakala tete ambayo imesainiwa kwa usahihi au barua ya maombi ikiwa kutakuwa hakuna mabadiliko yoyote ya akaunti ya benki ya mwekezaji ambayo haitakuwa tofauti na iliyo kwenye kumbukumbu ya Msimamizi wa Mfuko.

9.13. KIGEZO – HATI FUNGANI ZA SERIKALI ZA MIAKA MIWILI

Faida za Mfuko zitalinganishwa na Hati Fungani za Serikali za miaka miwili zilizopo kwenye soko. Kigezo hiki kinaweza kubadilishwa na Msimamizi wa Mfuko endapo mabadiliko yanayokusudiwa yatawasilishwa kwa wawekezaji.

10. MASHARTI YA KUJIUNGA NA MFUKO WA FAIDA

Mwekezaji mwenye sifa na nia ya kushiriki katika mfuko huu anatakiwa afuate masharti yafuatayo:-

- a) Kujaza fomu ya ununuzi wa vipande kama inavyoelezwa na Meneja wa Mfuko (kujaza Fomu mtandaoni kupitia Tovuti ya WHI au simu za mkononi). Unaweza pia kupakua Fomu kupitia kwenye tovuti ya WHI ambayo ni www.whi.go.tz
- b) Kulipa kiasi stahiki kinachotakiwa kwa kujiunga.

11. SERAYA UWEKEZAJI (INVESTMENT POLICY)

- a) Mfuko umelenga kufanya uwekezaji katika maeneo yenye kutoa athari ndogo za uwekezaji na wenye kukidhi mahitaji ya mwekezaji kwa haraka; hivyo uwekezaji katika soko la Hisa kuwa si sehemu ya uwekezaji wa mfuko.
- b) Kutokana na hilo, mgawanyo wa rasilimali kulingana na Sera ya Uwekezaji ya Mfuko umelenga katika maeneo yafuatayo:
- i) Uwekezaji kwenye masoko ya fedha - kwa kiwango kisizidi asilimia 40% ya Mfuko
- ii) Uwekezaji wenye kutoa Riba – Kwa kiwango kisichopungua asilimia 60% ya Mfuko. Uwekezaji kwenye masoko ya fedha ni aina ya uwekezaji ambao ukomo wake si zaidi ya Mwaka mmoja, wakati Uwekezaji wenye kutoza riba unahusu uwekezaji wenye kutoza viwango maalum vya riba katika kipindi kisichopungua mwaka mmoja kama vile Hati fungani za serikali, Dhamana za Serikali, Akiba Maalumu katika mabenki, Dhamana za mashirika zilizo rodheshwa katika soko la mitaji n.k.
- c) Kubadilisha Uwiano wa Uwekezaji wa Rasilimali za Mfuko: Uwiano wa mgawanyo wa uwekezaji wa rasilimali za Mfuko uliotajwa hapo juu unaweza kubadilishwa wakati wowote lengo likiwa ni kukidhi mahitaji ya soko, kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kisera na kisiasa pamoja na kunufaika na fursa mbalimbali zinazoweza kujitokeza. Ni vema ieleweke kwamba viwango vilivyotajwa hapo juu ni mwongozo tu,

Meneja wa mfuko anaweza kubadilisha wakati wowote pale atakapoona inafaa kufanya hivyo ili kulinda maslahi ya wawekezaji. Hakuna badiliko lolote litakalofanywa bila ya idhini toka Mamlaka inayosimamia soko la Mitaji na Dhamana (CMSA). WHI inawajibika kuomba kibali cha kufanya mabaliko hayo toka kwa Msimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ndani ya kipindi cha wiki tatu kabla ya utekelezaji.

Kumbuka: Sheria inoyosimamia Dhamana nchini Tanzania hairuhusu Mfuko wa Faida kukopa.

12. KUWEKA REHANI VIPANDE KAMA DHAMANAYA MKOPO

- a) Vipande vya Mfuko wa Faida vinaweza kutumika kama rehani kwa ajili ya kupata mkopo toka kwenye taasisi za fedha.
- b) Uwekaji wa rehani kwa ajili ya dhamana ya mkopo utafuata utaratibu unaotolewa na WHI pamoja na Taasisi za Fedha.
- c) Endapo taratibu za urejeshaji wa mkopo zitakiukwa, benki au taasisi ya fedha ina haki ya kuuza vipande kwa Msimamizi kwa ajili ya kulipia mkopo ilioutoa.
- d) Mwekezaji hana haki ya kuuza au kuhamisha vipande vilivyowekwa rehani isipokuwa kwa idhini toka benki au taasisi iliyotoa mkopo.

13. KUBADILISHA/KUHAMISHA WAMILIKI WA VIPANDE

Mfuko wa Faida unatoa fursa ya kubadilisha Umiliki wa vipande toka mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine.

Mabadiliko hayo yanaweza kufanyika katika mazingira yafuatayo :

- a) Mabadiliko ya kawaida (hii ni pale mmiliki mmoja anapoamua kuhamishia umiliki wake kwenda kwa mtu au Taasisi nyingine na kwamba mabadiliko haya si ya kibiashara).
- b) Mabadiliko ya Umiliki Kibiashara (hii ni pale mmiliki wa vipande anapoamua kuuza vipande vyake kwa mtu ama taasisi nyingine)
- c) Kuhamisha vipande vilivyowekwa rehani toka kwa mkopaji kwenda kwa Taasisi iliyotoa mkopo. Hayo yatafanyika endapo mmiliki wa vipande atashindwa kutimiza masharti ya mkopo aliochukua.
- d) Mabadiliko yatokanayo na kesi za mirathi na;
- e) Mabadiliko mengine yeyote stahiki kama vile amri ya Mahakama

Kumbuka:

- i) Kuhamisha sehemu ya umiliki (partial transfer) inaruhusiwa.
- ii) Hairusiwi kuhamisha/kubadilisha umiliki wa vipande kwa namna nyingine kinyume na yaliyoainishwa hapo juu.

14. MAUZOYAVIPANDE (ALLOTMENT OF UNITS)

- a) Mauzo ya awali ya vipande vitauzwa kwa bei ya Tsh 100/= kwa kila kipande. Uwekezaji wa nyongeza vipande vitanunuliwa kwa thamani halisi ya bei ya wakati huo.

- b) Vipande vitatolewa kwa tarakimu 4 za desimali.
- c) Mgao wa vipande utatolewa kulingana na kiasi kilichowekezwa kwa Meneja pamoja na kutimiza masharti yote kama yalivyoainishwa na Waraka wa Makubaliano.
- d) Taarifa ya akaunti itatolewa kila wakati mwekezaji anapofanya uwekezaji.

15. TAARIFA YA AKAUNTI (SOA)

- a) Taarifa ya akaunti itatolewa kwa kila manunuzi na mauzo ya vipande vya mfuko. Taarifa hiyo ya akaunti itaonyesha nambari ya akaunti ya uwekezaji, tarehe ya kupokea maombi ya mauzo / manunuzi, kiasi kilichowekezwa, bei ya mauzo/manunuzi na idadi ya vipande vilivyobakia kwenye akaunti ya mwekezaji.
- b) Mwekezaji atapatiwa taarifa ya akaunti ndani ya siku 1 ya kazi toka tarehe ya kupokea maombi ya mauzo/manunuzi. Hata hivyo taarifa ya akaunti itatolewa ndani ya siku tatu mara baada ya maombi kuwasilishwa Ofisi za Watumishi Housing Investments.
- c) Kwa wale wawekezaji watakojiunga na Mfuko wa FAIDA wakati wa kipindi cha mauzo ya awali taarifa ya akaunti itatumwa kama ilivyoainishwa katika kifungu 9.2(d) cha waraka huu.

16. UTEUZI WA MWAKILISHI/MRITHI

- a) Uteuzi wa mwakilishi/mrithi unaruhusiwa katika Mfuko huu.

- b) Pale ambapo vipande vinamilikiwa na watu zaidi ya mmoja katika umiliki wa pamoja au katika utaratibu wa “mmojawapo katika wamiliki” wanayo haki ya kuchagua mwakilishi/mrithi wa vipande vyao ambaye atakuwa na haki ya umiliki pale ambapo wawekezaji hao watakapokuwa wamefariki
- c) Wamiliki wasio watu binafsi hawawezi kumchagua mwakilishi/ mrithi.
- d) Suala la usimamizi wa vipande kwa niaba ya mtu litakoma punde vipande vitakapouzwa.
- e) Mwakilishi/Mrithi anaweza kuondolewa na wanaomiliki vipande na ambao mwanzo walimteua. Pale ambapo mwakilishi ameondolewa, Msimamizi hana wajibu wa kuhamisha vipande kwenda kwa mwakilishi.
- f) Ni mtu mmoja tu ambaye ni mkazi au ambaye sio mkazi pamoja na watoto(akiwakilishwa na mzazi/ mlezi) anaweza kuchaguliwa kuwa mrithi kama ilivyo kwenye fomu ya maombi
- g) Wakati wa kumwandikisha mwakilishi, taarifa ya akaunti katika barua maalumu itakayoamuliwa na Msimamizi wa Mfuko.
- h) Mwakilishi au Mrithi anaweza kubadilishwa na mwekezaji katika kipindi chote cha uwekezaji.
- i) Endapo mmiliki wa vipande amefariki na uteuzi wa mrithi umefanyika kwa kufuata taratibuzilizowekwa, vipande vitamilikishwa kwa mrithi kwa kuzingatia sheria na kanuni.

- j) Uteuzi wa Mwakilishi/Mrithi wa Mfuko utazingatia sheria za nchi. Hii inamaanisha kwamba Msimamizi hatakuwa na ruhusa ya kumpatia haki mtu mwingine yeyote ambaye hakuteuliwa kisheria.
- k) Itakapotokea mgogoro baina ya warithi inayopelekea mashitaka mahakamani, maamuzi ya Mahakama yatazingatiwa. Uteuzi wa uwakilishi katika Mfuko huu sio wa mwisho.

17. UNUNUZI WAVIPANDE

16.1. WAKATI GANI UNUNUZI WAVIPANDE UNAFANYIKA

- a) Vipande vinaweza kununuliwa muda wowote katika masaa 24 ya siku; wakati wa mauzo ya awali na mauzo yanayofuata. Utaratibu wa mauzo umeainishwa kwenye Kiambatishi.
- b) **Kumbuka**
- i) Fomu za maombi za ununuzi wa vipande pamoja na Waraka wa Toleo zinapatikana kwa Wakala au kupitia kwenye tovuti ya WHI: www.whi.go.tz. Maombi ya ununuzi wa vipande unaweza kufanyika mtandaoni (kupitia Tovuti ya WHI au simu za mkononi).
- ii) Wawekezaji wanaruhusiwa kuwasilisha maombi zaidi ya mara moja katika kipindi cha mauzo ya awali.

17.2. UPATIKANAJI WAVIPANDE

Wakati wa kipindi cha mauzo ya awali pamoja na mauzo yanayofuata,

vipande vya Mfuko huu vinaweza kupatikana kama ifuatavyo:

- a) Kwa kupitia mtandaoni katika Mfumo katika Tovuti ya WHI au simu za mkononi (USSD, Faida Fund App).
- b) Matawi yote ya Benki za CRDB na benki nyingine za biashara.
- c) Huduma kwa Wateja katika Ofisi zote za Watumishi Housing Investments.
- d) Ofisi zote za Madalali na Wakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam

17.3. MALIPO KWA AJILIYA UNUNUZI NA UUZAJI WAVIPANDE

Sarafu itakayotumika ni shilingi ya Tanzania (Tsh) tu. Malipo yatafanyika kwa fedha taslimu (shilingi ya Kitanzania) au uhamisho wa Benki kwenda akaunti ya makusanyo ya Mfuko wa Faida iliyopo katika Benki ya CRDB.

Malipo yatafanyika (kupitia namba ya malipo aliyopewa mwekezaji wakati wa kujiunga) kwa njia ya uhamisho wa kibenki kwenda kwenye akaunti ya mwekezaji baada ya Msimamizi kupokea taarifa za kibenki au simu pesa ya mwekezaji.

Wawekezaji kutoka nchi nyingine wanaweza kujiunga kwa njia ya mtandao (Tovuti ya WHI au simu za mkononi) au kutumia Waangalizi au Mawakala walioorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Vile vile, wanaweza kuwasiliana kwa barua pepe faidafund@whi.go.tz

Kumbuka: Hakuna Fedha taslimu/Hundi inayohusiana na akaunti ya Mfuko ya ununuzi wa vipande kulipwa kupitia taasisi nyingine yoyote tofauti na

akaunti ya makusanyo ya Mfuko wa Faida iliyopo Benki ya CRDB.

18. MAUZOYANAYOFUATA NA UUZAJI WAVIPANDE KWA MSIMAMIZI

18.0.1. MAUZOYANAYOFUATA

Mauzo yanayofuata baada ya mauzo ya awali ya vipande vya Mfuko yataanza rasmi mara baada ya kumalizika kwa kipindi cha mauzo ya awali. Kutoka mud huo, Msimamizi (WHI) ataendelea kuuza vipande kulingana na thamani halisi ya vipande (NAV) ya siku husika. Utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:

- a) Uuzaji wa vipande utafanyika kutegemea thamani ya vipande ya wakati huo bila gharama kulingana na vigezo vilivyoko kwenye Waraka wa Toleo;
- b) Wawekezaji wanashauriwa kuangalia thamani halisi ya vipande vya Mfuko wa Faida pindi wanapotafakari kununua vipande. Endapo watakuwa na mashaka, wawekezaji wanashauriwa kupata ushauri wa kitaalam;
- c) Endapo Mwekezaji amefanya maamuzi ya kununua vipande, afuate taratibu zilizoainishwa kwenye Kiambatishi kwenye Waraka huu;
- d) Mwekezaji atajaza fomu ya maombi ya ununuzi wa vipande vya Mfuko wa Faida kwa njia ya mtandao au kujaza Fomu;
- e) Baada ya kuwasilisha Fomu ya maombi mwekezaji atapewa numba

ya malipo ya uwekezaji ya kudumu. Atatumia namba hiyo kufanya malipo ya ununuzi wa vipande.

- f)** Maombi ya malipo ya ununuzi wa vipande yanayofuata yatahesabika yamepokelewa na kukubaliwa na Msimamizi wa vipande saa za kazi (yaliyopokelewa kabla ya saa 10:00 jioni) za siku husika. Endapo yatapokelewa baada ya saa 10:00 jioni, yatahesabika siku ya kazi inayofuata;
- g)** Maombi yote ya mauzo ya vipande yanayofuata yaliyopokelewa na kukubaliwa kwa siku husika, yatazingatia thamani halisi ya vipande ya siku inayofuata;
- h)** Mkataba wa mauzo ya vipande utahesabika kuwa umekamilika baada ya maombi kukubaliwa isipokuwa tu kama maombi yatakataliwa na Msimamizi;
- i)** Kwa mauzo ya vipande baada ya mauzo ya mwanzo, mwekezaji atapata taarifa ya akaunti yake ambayo itatumwa kwake si zaidi ya siku moja kutoka siku ya kupokelewa maombi.

18.1. MANUNUZIYA NYONGEZAYAVIPANDE

Mauzo ya nyongeza ya vipande kwa mwekezaji aliyekwisha wekeza yatafanyika wakati wowote kwa kutimiza masharti ya uwekezaji wa nyongeza ya kulipa kiasi kisichopungua Tsh 5000/=.

18.2. UUZAJI WAVIPANDE KWA MSIMAMIZI

Uuzaji wa vipande kwa Msimamizi wa Mfuko utaanza miezi mitatu baada ya kumalizika kipindi cha mauzo ya awali. Kuanzia tarehe hii na kuendelea, msimamizi anaweza kununua vipande kutoka kwa wawekezaji.

Utaratibu wa mauzo ya vipande vya Mfuko kwa Meneja utakuwa kama ifuatavyo:

- a) Uuzaji wa vipande utafanyika kwa kuzingatia bei ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote;
- b) Wawekezaji wanashauriwa kuzingatia thamani halisi ya kipande wakati wanapotafakari kuuza vipande kwa Watumishi Housing Investments. Iwapo watakuwa na mashaka wanashauriwa kufuata ushauri wa kitaalam kutoka kwa wataalam wa masuala ya fedha;
- c) Itakapotokea kuwa mwekezaji yeyote anaamua kuuza vipande anapaswa atume maombi kwa njia ya mtandao au aende katika ofisi za Watumishi Housing Investments au wakala wake ambako atapewa fomu ya maombi ya kuuza baadhi ya vipande na taarifa nyinginezo;
- d) Mwekezaji atapaswa ajaze fomu ya maombi ya kuuza vipande vya Mfuko wa Faida kwa njia ya mtandao au kujaza Fomu;
- e) Fomu ya maombi ipelekwe katika ofisi ya Watumishi Housing Investments au wakala wake ikiwa;

- f) Maombi yatachukuliwa kuwa yamepokelewa siku husika iwapo yatawasilishwa katika ofisi ya Watumishi Housing Investments au wakala wake katika masaa ya huduma za kibenki katika siku za kazi (kabla ya saa 10 alasiri);
- g) Maombi ya mauzo ya vipande yatakayopokelewa katika ofisi ya Watumishi Housing Investments au wakala wake yatumia thamani ya kipande ya siku ya kazi inayofuata;
- h) Mauzo ya vipande yatakayopokelewa katika ofisi ya Watumishi Housing Investments yatashughulikiwa ndani ya siku tatu za kazi na fedha zitatumwa moja kwa moja kwenye akaunti ya mteja iliyoandikishwa au simu ya mkononi iliyosajiliwa;
- i) Pale ambapo fedha zitarudishwa baada ya kutumwa kwa njia ya benki mwenye vipande hatadai fidia yoyote kutokana na kuchelewa kwa malipo yake.

19. MASHARTI YA UWEKEZAJI KWA WASHIRIKA

Watumishi Housing Investments haitawekeza katika Mfuko wa Faida.

20. MAONI NA MALALAMIKO YA WAVEKEZAJI

- a) Msimamizi wa Mfuko anaamini katika kutoa huduma bora na zenye ufanisi kwa wawekezaji ili kumfanya mwekezaji awe mwenye uzoefu wenye tija katika uwekezaji kwenye mfuko huu. Ili kutimiza malengo haya, Msimamizi amebobea katika uanzishwaji na uboreshwaji wa mifumo

ili kutoa huduma bora na kushughulikia matatizo mbalimbali ya wateja kwa wakati.

Kama kuna maoni au malalamiko yoyote juu ya uendeshaji wa mfuko huu, tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:-

Mkuregenzi Mtendaji, Watumishi Housing Investments,

Jengo la Golden Jubilee, Ghorofa ya 4,

7 Mtaa wa Ohio/Kibo,

S.L.P 5119, 11481 Dar es Salaam,

Simu: +255 22 2922211,

Nukushi: +255 22 2922221

Barua pepe: wekeza@whi.go.tz

Tovuti: www.whi.go.tz

b) Watumishi Housing Investments inaweza kuteua Afisa Uhusiano wa Wawekezaji ndani ya Mfuko.

Kumbuka: Fomu maalum ya malalamiko ya Wawekezaji inapatikana katika Ofisi na tovuti za Msimamizi/Mwangelizi wa Mfuko.

c) Itakapotokea mwekezaji kutoridhishwa na majibu ya Msimamizi, basi anaweza kufikisha malalamiko yake katika Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa maamuzi. Endapo mwekezaji au Msimamizi

hataridhika na majibu/maamuzi ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, basi watakuwa huru kwenda mahakamani.

21. GHARAMA ZA MFUKO

Gharama zifuatazo zitalipwa kutokana na mapato ya Mfuko:

- a) Kodi kulingana na viwango vya kodi vinavyotumika;
- b) Ada zote kama zitakavyoelekezwa na taasisi husika kama vile Soko la Hisa;
- c) Ada ya ushauri wa uwekezaji ya asilimia 1.8 ya thamani halisi ya mfuko kwa mwaka.
- d) Ada ya Mwangalizi wa Mfuko itatozwa kiasi kisichozidi asilimia 0.1 ya thamani halisi ya Mfuko kwa mwaka ilimradi ukomo usiwe chini ya shilingi milioni tano (Tsh 5,000,000/=).
- e) Gharama nyinginezo ni asilimia 0.60 ya thamani halisi ya Mfuko kwa mwaka. Hii inajumuisha gharama za kawaida katika uendeshaji wa shughuli za kila siku kama vile:
 - i) Gharama za kuuza/uwakala pamoja na matangazo.
 - ii) Gharama za Benki
 - iii) Gharama za ukaguzi wa hesabu iv) Gharama za mwanasheria
- v) Gharama zinazohusiana na uuzaji na ununuzi wa vipande

vi) Gharama zinazohusiana na huduma kwa wawekezaji.

Hata hivyo gharama nyiingine na gharama za ushauri wa uwekezaji kama zilivyoainishwa hapo juu zitakuwa na ukomo wa asilimia 2.50 ya thamani halisi ya Mfuko. Katika hali ambayo gharama zitazidi asilimia 2.50 ya thamani halisi ya Mfuko basi kiasi kitakachozidi kitalipwa na Msimamizi wa Mfuko.

Vile vile ikumbukwe kwamba gharama zote za mauzo ya awali zitagharimiwa na Msimamizi wa Mfuko na kwa mauzo ya baadaye zitagharimiwa na Mfuko wenyewe.

Makisio ya gharama za awali yameainishwa kama ifuatavyo:

- i) Gharama za matangazo na masoko.
- ii) Gharama za Ushauri.
- iii) Gharama za Posta na Uchapishaji.
- iv) Gharama za mwanasheria/ukaguzi wa hesabu.
- v) Gharama nyinginezo.

Gharama zote za awali zitagharimiwa na Msimamizi ambaye pia ni mdhamini wa Mfuko.

22. JINSIYA KUTATHMINI THAMANI HALISIYA MFUKO

a) Thamani halisi ya Mfuko, itapatikana kwa kuthaminisha rasilimali zote

za Mfuko na kutoa madeni yote baada ya kuzingatia mapato ambayo yanajulikana lakini hayajapokelewa na gharama zinazokisiwa. Thamani halisi ya kipande itatafutwa kwa kugawanya thamani halisi ya rasilimali zote za Mfuko kwa idadi ya vipande kwa wakati huo.

- b) Watumishi Housing Investments itatangaza thamani halisi ya Mfuko katika siku zisizozidi 10 tangu kufungwa kwa mauzo ya awali. Baada ya hapo itatangazwa kila siku kama ifuatavyo:
- i) Thamani halisi ya kipande itatolewa katika vyombo vya habari kwa kutangazwa katika kila siku ya kazi.
 - ii) Thamani halisi ya kipande itatangazwa katika magazeti yanayosomwa kwa wingi nchini.
 - iii) Thamani halisi ya kipande itakuwepo pia katika tovuti ya Watumishi Housing Investments (www.whi.go.tz).
 - iv) Iwapo katika siku yoyote ya kutathimini thamani ya Mfuko na endapo Soko la Hisa la Dar es Salaam litakuwa limefungwa kwa sababu ya sikukuu au sababu nyingine yoyote, bei za siku iliyotangulia zitachukuliwa kama ndio thamani halisi ya kipande/ mfuko.

23. HAKI ZA WAMILIKI WAVIPANDE

- a) Haki ya kufaidika na rasilimali za Mfuko na mtawanyo wa vipande kulingana na walichowekeza katika Mfuko.

- b) Wenye vipande wanayo haki ya kuiomba Watumishi Housing Investments habari yoyote ambayo inaweza kuwa na matokeo mabaya juu ya rasilimali zao, na Watumishi Housing Investments itawajibika kutoa habari hiyo kwa wamiliki hao.
- c) Muhtasari wa Taarifa ya Mwaka kuhusu maendeleo ya Mfuko utatumwa kwa wenye vipande, siyo zaidi ya miezi minne tangu tarehe yakufungwa kwa mwaka wa fedha husika, na utakuwa tayari kwa kukaguliwa katika ofisi za Watumishi Housing Investments na matawi ya Benki ya CRDB ambayo ni Mwangalizi wa Mfuko.
- d) Taarifa za mwaka wa fedha wa Mfuko utaishia tarehe 30 Juni kila mwaka
- e) Mabadiliko yoyote katika vipengele muhimu vya Mfuko yatafanywa pale tu wenye vipande watakapoamua kutoka kwenye Mfuko kuruhusiwa kuuza vipande vyao kwa bei ya thamani halisi ya kipande kwa wakati huo. Wenye vipande watajulishwa kupitia matangazo kwenye magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchini kote.
- f) Wenye vipande wanayo haki ya kukagua nyaraka zifuatazo katika ofisi ya Watumishi Housing Investments:-
 - i) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 (kama ilivyorekebishwa).
 - ii) Taratibu/Kanuni za mipango ya Uwekezaji wa pamoja za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1997.

- iii) Waraka wa Makubaliano wa Mfuko wa Faida. iv) Waraka wa Toleo wa Mfuko wa Faida;
- v) Sheria ya Uanzishwaji wa Dhamana ya Uwekezaji Namba 318.

24. KODI

Maelezo yafuatayo ni kwa taarifa za jumla kwa wawekezaji. Taarifa sahihi kuhusu mambo ya kisheria na kodi, kila mwekezaji anashauriwa kupata ushauri wa mwanasheria au mshauri wa kodi.

Kulingana na sheria ya kodi inayotumika wakati wa kutoa Waraka wa Toleo hili, kodi zitakazotowazwa zitakuwa kama ifuatavyo:-

- a) Mapato ya Mfuko yatoakanayo na riba yatatozwa kodi ya zuiyo ya asilimia 10% ambayo itakuwa ni kodi ya mwisho (Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004);
- b) Mapato yatoakanayo na Hati Fungani za Serikali yenye kuiva zaidi ya kipindi cha miaka miwili hayatatozwa kodi (Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004);
- c) Ongezeko la thamani kwenye hisa zilizoordheshwa kwenye Soko la Hisa Dar Es Salaam na Hati Fungani za Serikali zenye kumilikiwa na Mfuko, hazitatozwa kodi (Income Tax Act 2004 - 2nd schedule f (i)- (vi)).

25. UKOMO KWA MFUKO

- a) Mfuko unaweza kufikia ukomo:

- i) Iwapo itaamuliwa hivyo kwenye Mkutano Mkuu usio wa kawaida wa Wawekezaji;
- ii) Iwapo ukomo utakuwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 122 na 124 cha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

26. MAMBOYA JUMLA

- a) Maombi ya kununua vipande katika mazingira yafuatayo, yanaweza kukataliwa na Msimamizi endapo:
 - i) Maombi yamepokelewa pamoja na fedha pungufu ya kima cha chini kinachoruhusiwa kwa ajili ya kununua vipande.
 - ii) Fomu ya maombi haikutiwa saina na mwombaji.
 - iii) Mwombaji hana sifa za kuwekeza katika Mfuko huu.
 - iv) Ikiwa Meneja hakupokea malipo kutokana na hundi iliyowasilishwa kwa ajili maombi kukataliwa na benki.
- b) Uamuzi wowote wa Watumishi Housing Investments kuhusu kustahili au kutostahili kwa mwombaji kujiunga na Mfuko, utakuwa ni wa mwisho baada ya kuthibitishwa na Mamlaka. Kurejeshwa kwa fedha za maombi yaliyokataliwa utafanyika baada ya taratibu za kiutendaji kutekelezwa kwa gharama ya mwombaji na Msimamizi hatawajibika kulipa riba au kiasi kingine chochote cha fedha.

- c) Wamiliki ambao umiliki wao unatokana na udanganyifu katika maelezo yao, utafutwa na majina yao kuondolewa katika Daftari (Kanzi data) la wenye vipande. Katika hali kama hiyo, Msimamizi atakuwa na haki ya kununua tena umiliki wa vipande hivyo kwa bei ya mwanzo au thamani halisi ya kipande ya wakati huo kutegemea bei ipi itakuwa ndogo kati ya hizo, baada ya kutoza kiasi ambacho ni sawa na asilimia kumi (10%) ya bei ya kununua kama adhabu. Msimamizi anaweza kuchukua mgawanyo wa mapato, kama upo, ambao ulilipwa kwa wenye vipande wa namna hiyo kwa makosa na kulipa kiasi hicho kwa mwekezaji anayestahili.

27. MIKUTANO

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa wawekezaji kila mwaka kama ifuatavyo:

- a) Mwekezaji ataruhusiwa kuwakilishwa;
- b) Pia kunaweza kutokea kuitishwa kwa Mkutano Mkuu usio wa kawaida (Extraordinary General Meeting).



KIAMBATISHI NA. – FOMU YA MAOMBI



**WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS
FAIDA FUND UNIT TRUST SCHEME
INDIVIDUAL & JOINT REGISTRATION FORM**



TYPE OF INVESTMENT/ AINA YA UWEKEZAJI

Individual Investment/ Mwekezaji Binafsi Minor Investor/ Mtoto chini ya Miaka 18.
 Joint Investment/ Uwekezaji Shirikishi

Attach Passportsize
Weka picha

SECTION A - INDIVIDUAL INVESTORS

INVESTORS INFORMATION

Name/ Jina	Date of Birth/ Tarehe ya kuzaliwa	Identity card type/ Aina ya kitambulisho
Identity card number/ Namba ya kitambulisho		
Adress/ Mawasiliano		
Phone Number/ Namba ya simu	Email/ Barua pepe	Nationality/ Utaifa
Region of Residence/ Mkoa unapoishi	District of residence/ Wilaya unapoishi	Physical Address/ Anwani ya Makazi
Postal Address/ Sanduku la posta		

Bank Details

Bank Account Number/ Namba ya akaunti ya Benki	Bank Name/ Jina la Benki	Bank Branch/ Tawi la Benki
Bank Branch Region/ Tawi la Benki		
Next of Kin		
Name/ Jina	Mobile Number/ Namba ya simu	Email/ Barua Pepe
Postal Address/ Sanduku la Posta	Relationship/ Mahusiano	

SECTION B - JOINT INVESTORS

INVESTORS INFORMATION

Partner Basic Details

Name/ Jina	Date of Birth/ Tarehe ya kuzaliwa	
Identity card type/ Aina ya Kitambulisho	Identity card Number/ Namba ya kitambulisho	Fund Name/ Jina la Mfuko

Attach Passportsize
Weka picha

Partner Address Details

Phone Number/ Namba ya Simu	Email Address/ Barua pepe	Nationality/ Utaifa
Region of residence/ Mkoa unapoishi	District of Residence/ Wilaya unapoishi	Physical Address/ Anwani ya Makazi
Postal Address		

Bank Details

Bank Account Number/ Namba ya akaunti	Bank Name/ Jina la Benki	Bank Branch/ Tawi la Benki
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
Bank Branch Region/ Mkoa lilipo tawi la Benki		
<input type="text"/>		

Next of Kin

Name/Jina	Mobile Number/ Namba ya simu	Email/Barua pepe
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
Postal Address/ Anwani ya Makazi	Relationship/ Mahusiano	
<input type="text"/>	<input type="text"/>	

SECTION C - MINOR INVESTOR

INVESTORS INFORMATION

Name/Jina	Date of Birth/ Tarehe ya kuzaliwa	Attach Passportsize Weka picha
<input type="text"/>	<input type="text"/>	
Phone Number/Namba ya simu	Email/ Barua pepe	Nationality/ Utaifa
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

Please attach (i) Passportsize (ii) national identity card or any proof of your nationality (For all Applicants)

SEHEMUYA KWANZA: MAELEKEZO YA JUMLA

1. Tafadhali rejea taarifa zilizotolewa kwenye waraka watoleo.

Mwombaji awasiliane (kama atahitaji) na ofisi ya mawakala wa waliosajiliwa wa soko la hisa la Dar es Salaam, meneja wa benki, mhasibu, wataalam na washauri wa masuala ya Uwekezaji au mwanasheria atakapojaza Fomu ya maombi ya kujiunga

2. Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya mwanzo kuanzia tarehe 01 Novemba mpaka 30 Disemba 2022

3. Jaza taarifa zote kwa kutumia HERI KUBWA. Maombi yanafanywe Kwa njia ya mtandao au kwenye fomuhalisi.

4. Wakati wa mauzo ya mwanzo, vipande vitauzwa kwa njia ya mtandao, katika ofisi za WHI na ofisi za mwakala zifuatazo:

a. Matawi yote ya Benki ya CRDB

b. Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam.

5. Kumbuka, usitoe pesa kwa mtu yeyote asiye wakala aliyeteuliwa, na baada ya kukabidhi pesa na fomu ya maombi hakikisha unapata risiti kutoka kwa wakala aliyepokea maombi yako na fedha ikionyesha namba yako ya malipo.

6. Maombi katika mtandao au kwa kujaza Fomu yatakamilika baada ya kupokelewa malipo ya uwekezaji kwenye akaunti ya “mfuko wa faida”.

7. Mabadiliko yoyote katika fomu ya maombi yadhhibitishwe kwa saina kamili ya mwombaji.

8. Maombi yote yakishawasilishwa hayatarudishwa bali yatashughulikiwa kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye waraka watoleo.

10. Baada ya mauzo ya mwanzo, wamiliki halali wa vipande watatumiwa taarifa ya akaunti kuonesha idadi ya vipande vya mfuko wanavyomiliki kupitia simu zao za mkononi zilizosajiliwa.

11. Mauzo ya baadae: Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya baadaye ya vipande mara baada ya tarehe ya mwisho ya mauzo ya awali.

SEHEMUYA PILI: MAMBO YA MUHIMU KUHUSU MFUKO WA FAIDA

i.	Malengo	Mfuko wa wazi wa kukua kwa mtaji ambao unawezeza katika soko la fedha kwenye amana na hatifungani za serikali Mfuko una lengo la kukua mtaji wa wawekezaji kulingana na faida itakayopatikana.
ii.	Sera ya Uwekezaji	Uwekezaji itakuwa katika uwekezaji unatoa faida isiyobadilika. Zaidi ya asilimia sitini katika uwekezaji wenye kutoza riba na Chini ya asilimia arubaini itawekezwa katika masoko ya fedha ili kutoa urahisi wa kubadilishwa katika fedha taslimu kwa ajili ya kuwalipa wanaouza vipande.
iii.	Mpango wa Uwekezaji	Mfuko unampango mmoja tu wa Uwekezaji ambao ni kukua kwa mtaji
iv.	Wawekezaji wanaoruhusiwa	Wawekezaji wote ikiwa ni pamoja na watu binafsi na taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Kanuni zinazoambatana na Sheria hiyo.
v.	Thamani ya mwanzo ya kipande	Shilingi 100/=
vi.	Bei ya kipande	Bei ya kipande katika mauzo ya mwanzo yatakayofanyika kuanzia 01 Novemba 2022 hadi tarehe 30 Disemba 2022 ni Shilingi 100.
vii.	Gharama za kujiunga na kujitoa kwenye mfuko	Hakutakuwa na gharama za kujiunga wala kujitoa kwenye mfuko. Mwekezaji atanunua vipande kwa thamani au kuuza vipande kwa thamni halisi ya kipande kwa siku hiyo..
viii.	Kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza	Shilingi 10,000/=

FAIDA FUND

ix.	Kiwango cha chini cha Uwekezaji wa nyongeza	Shilingi 5,000/=
x.	Kiwango cha juu cha Uwekezaji	Hakuna kiwango cha juu / Ukomo wa uwekezaji.
xi.	Umiliki wa vipande	Umiliki wa mtu mmoja mmoja au umiliki wa pamoja kwa watu binafsi.
xii.	Utaratibu wa kuwekeza	Mwekezaji anatakiwa kujaza na kukamilisha Fomu ya Maombi ya Kujiunga na Mfuko kwa njia ya mtandao au kujaza Fomu na kuweka fedha kwa kutumia namba ya malipo ya uwekezaji (aliyopewa wakati wa usajili) katika akaunti ya Mfuko ya makusanyo iliyop benki ya CRDB.
xiii.	Masharti ya malipo	Malipo yote yanatakiwa kufanyika kikamilifu kwa idadi maalumu ya vipande vilivyoombwa.
xiv.	Uwekezaji wa nyongeza	Wawekezaji wanaweza kufanya uwekezaji wa ziada baada ya kipindi cha mauzo ya awali. Kiwango cha chini cha uwekezaji wa ziada ni Shilingi 5,000/=.
xv.	Ukwasi/kuuza vipande	Baada ya mauzo ya mwanzo, bei ya kununua na kuuza kipande itategemea thamani halisi ya kipande katika Mfuko kwa wakati huo (NAV). Mfuko hautatoza gharama yeyote ya kujiunga au kujitoa katika mfuko.
xvi.	Uwazi	Tathmini ya thamani halisi ya Mfuko itakokotolewa kila siku ya kazi na thamani ya kipande kutangazwa.

xvii.	Faida za kodi	Kwa mujibu wa sheria za sasa, mapato kutoka katika uwekezaji kwenda kwa mwekezaji hayatozwi kodi ya mapato. Pia hakuna makato ya kodi wakati wa kuuza vipande. Sheria ya kodi ya ,mapato jedwali la pili (u)
xviii.	Thamani ya Kipande	Thamani halisi ya kipande itakuwa inatolewa na Meneja kila siku ya kazi baada ya saa 10 jioni kwa saa za Tanzania

JINSI YA KUJISAJILI NA KUWEKEZA

Mwekezaji ataweza kujisajili kwa kujaza fomu

au kwa njia ya mtandao.

1) Simu: USSD

Piga: *152*00#

Chagua: malipo

Chagua: FAIDA FUND

2) Simu: Simu janja

Pakua: Aplikesheni / Wekeza WHI

3) Tovuti: www.whi.go.tz

